

OFISI YA RAIS

TAWALAZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

MIKOA WA DAR ES SALAAM

MTIHANI WA UTAMILIFU - KIDATO CHA NNE 2024

KISWAHILI

MSIMBO 02

MUDA: MASAA 3:00

Alhamisi 11 Julai, 2024 Mchana

MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina sehemu **A, B na C** Zenye jumla ya maswali **kumi na moja (11)**
2. Jibu maswali **yote** katika sehemu A na B na maswali mawili (2) kutoka sehemu C
3. Sehemu A ina alama **kumi na sita (16)** sehemu B alama **hamsini na nne (54)** na sehemu C ina alama **thelathini (30)**
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na kila swali
5. Simu za mkononi na vitu vyote **visivyoruhusiwa** havitakiwi katika chumba cha mtihani
6. Andika **namba yako ya mtihani** katika kila ukurasa wa kitabu chako cha kujibia

Karatasi hii ina kurasa 5 zenye maandishi

SEHEMU A (Alama 16)

Jibu maswali yote

1. Chagua herufi ya jibu sahihi katika vipengele (i) hadi (x) kisha andika herufi ya jibu hilo katika karatasi ya kujibia
- i) Mzee Bukuku ana watoto watano, wanne wamebatizwa majina kutoka kwenye nomino za pekee na mmoja amebatizwa jina kutoka kwenye nomino dhahania. Je unafikiri mtoto wa mzee Bukuku ambaye ana jina la nomino dhahania atakuwa nani kati ya hawa?
- A. Januari
 - B. Faraja
 - C. John
 - D. Amosi
 - E. Masanja
- ii) Wewe ni mahiri wa lugha. Muoneshe rafiki yako mpangilio sahihi na mjengo wa Tungo.
- A. Neno, kishazi, sentensi na kirai
 - B. Kishazi, kirai, sentensi na Neno
 - C. Sentensi, Neno, Kishazi na kirai
 - D. Kirai, Neno, Sentensi na Kishazi
 - E. Neno, kirai, kishazi na sentensi
- iii) Ili mzungumzaji wa lugha aweze kuwasiliana kwa usahihi, anahitaji kuzingatia mambo muhimu manne ambayo ni
- A. Mahali, mada, muda, wahusika
 - B. Maudhui, lengo, mada, maana
 - C. Lengo, mada, mandhari, umbo
 - D. Mada, uhusiano, mandhari na lengo
 - E. Sifa binafsi, mada, maana, uhusiano
- iv) Clatus Chama alifanya zoezi la kupachika kauli katika mizizi ya vitenzi mbalimbali. Unafikiri Chama alifanya zoezi gani kati ya haya?
- A. Unyambulishaji
 - B. Unominishaji
 - C. Utendekaji
 - D. Akronomia
 - E. Uambatanishaji
- v) Waingereza walifanya mambo mbalimbali katika kukuza na kueneza lugha ya kiswahili ikiwemo kuunda kamati ya Inter - Territorial Language (swahili) Committee iliyo anzishwa mwaka
- A. 1940
 - B. 1830
 - C. 1930
 - D. 1822
 - E. 1922
- vi) Umepewa kazi ya kumfundisha kiswahili mgeni ambaye hajui kutumia kamusi ya lugha ya kiswahili, mfundishe kubainisha seti ya maneno inayofaa kuing'izwa kwenye kamusi kwa kuzingatia mpangilio wa Alfabeti
- A. Jabali, Jabiri, Jadhika, Jadi, Jalada
 - B. Jabali, Jadhika, Jabiri, Jadi, Jalada
 - C. Jabiri, Jabali, Jalada, Jadi, Jadhika
 - D. Jabali, Jadi, Jadhika, Jalada, Jabiri
 - E. Jabali, Jalada, Jabiri, Jadhika, Jadi
- vii) "Waandishi wa Tamthiliya mbalimbali huzungumzia watu wenye mienendo inayokubalika na isiyokubalika katika jamii". Katika tamthiliya ulizosoma ni wahusika wapi kati ya wafuatao wana mienendo isiyokubalika katika jamii ya mtanzania wa leo".
- A. John, Ngoswe na Mama Mazoea
 - B. Mazoea, Mama Furaha na Joti
 - C. Padri James, Ngoswe na Mama Anna
 - D. Ngoswe, Joti na Padri James
 - E. Padri James, Ngoswe na Mjomba

- viii) "Ngombe zangu wanatoa maziwa mengi." Kosa lililojitokeza katika tungo hii ni lipi kati ya haya?
- Udondoshaji wa herufi
 - Uongezaji wa kiambishi
 - Unyambulishaji wa maneno
 - Unyumbuaji wa maneno
 - Upatanisho wa kisarufi
- ix) Kushindana na mtu aliyekuzidi kila hali si busara"
- Methali zifuatazo zinashabihisha kauli hii isipokuwa
- Mwenye pesa si mwenzio
 - Chanda chema huvikwa pete
 - Mwenye nguvu mpishe
 - Nazi haishindani na jiwe
 - Maji yakija kasi yapishe
- x) Ni hatua ipi inafuata baada ya kipengele cha mwisho wa barua katika uandishi wa barua rasmi
- Jina la mwandishi
 - Saini ya mwandishi
 - Cheo cha mwandishi
 - Anuani ya mwandishi
 - Salamu za maagano

2. Oanisha manaa za vipera vya hadithi katika **orodha 'A'** na vipera vinavyohusika katika **orodha 'B'** kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi

ORODHA 'A'		ORODHA 'B'	
i)	Husimuliwa kama mifano ya kuadilisha watu	A:	Soga
ii)	Husimulia chimbuko la asili na ukweli wa mambo	B:	Tarihi
iii)	Husimuliwa kwa nia ya kuchekeka na kukejeli	C:	Vigano
iv)	Husimulia juu ya mhusika mmoja mjanja ambaye hunufaika kwa udanganyifu kutoka kwa mhusika	D:	Visasili
v)	Husimuliwa kwa lengo la kuwaasa watoto	E:	Ngano
vi)	Husimamulia matukio ya kihistoria	F:	Mizungu
		G:	Hadithi
		H:	Hekaya

SEHEMU B (Alama 54)

Jibu maswali yote katika sehemu hii

3. Kidato cha kwanza, mwalimu alikufundisha mada ya mawasiliano na kukujaza kwamba lugha ni nyenzo kuu ya mawasiliano. Kwa maarifa hayo, unaweza kusema lugha ni nini? na kueleza namna nne ambavyo unaweza kuilinda lugha ya kiswahili isitoweke.
4. (a) Eleza maana ya utata katika tungo
- (b) Kwa kila sentensi (i - iv) eleza sababu moja iliyosababisha utata huo
- Mama amenunua mbuzi
 - Mwajuma ametumwa na rama
 - Nimemjengea nyumba
 - Ally anaua
- (c) Tunga sentensi mbili katika kila sentensi moja uliyopewa ili kuondoa utata katika sentensi hiyo.
5. (a) Eleza maana ya kielezi
- (b) Eleza kwa ufupi mazingira manne ambayo kielezi huweza kujipambanua, kisha tunga sentensi moja kwa kila aina ya mazingira

4) "Ngonde zangu wanabwa naziwa mengi" Kuse iliyotokoeza katika lugha hii ni ipi?

- A. Jambisaji wa herufi
- B. Uongesaji wa kiamishi
- C. Umpambanaji wa maneno
- D. Umpambaji wa maneno
- E. Umpambaji wa kiswahi

5) Kuchinana na mtu aliyekuzidi kwa hali si busara"

Mtali aliyazidi mshabikiwa kauli hii isipokuwa

- A. Mwenye pesa si mwenzi
- B. Chana chena hufika pite
- C. Mwenye nguvu mishi
- D. Nani tashindani na jwe
- E. Maji yaka kesi yapishe

6) Taba pi nafuata baada ya kipegele cha mwisho wa hama katika uandishi wa hama rasmi

- A. Jira la mwandishi
- B. Saini ya mwandishi
- C. Chio cha mwandishi
- D. Anuani ya mwandishi
- E. Salamu za magano

7) za vipera vya hadithi katika orodha 'A' na vipera vinavyochusika kwa kuthaga herufi ya jibu sahihi

A: kama niifano ya kuadilisha watu
B: kimbuko la asili na ukweli wa mambo
C: kwa rila ya kuchekesha na kukejeli
D: ya mhusika mmoja mjanja ambaye
E: udanganyifu kutoka kwa mhusika
F: lengo la kuwasa watoto
G: tukio ya kihistoria

ORODHA 'B'

- A: Soga
- B: Tarihi
- C: Vigano
- D: Visasili
- E: Ngano
- F: Mizungu
- G: Hadithi
- H: Hekaya

SEHEMU 8 (Alama 54)

Swali yote katika sehemu hii

alikufundisha mada ya mawasiliano na kukujaza kwamba
lano. Kwa maarifa hayo, unaweza kusema lugha ni nini?
unaweza kuilinda lugha ya kiswahili isitoweke.

tungo
sababu moja iliyosababisha utata huo

ama
ensi moja uliyopewa ili kuondoa utata katika
ielezi huweza kujipambanua, kwa

6. "Mara nyingi babu hutusimulia hadithi wakati wa jioni, hadithi ni moja ya tanzu za fasihi simulizi" Fafanua kwa hoja sita mambo yanayoipa uhai fasihi simulizi
7. Kwa kutumia mifano kutoka katika riwaya ya Takadini iliyoandikwa na Ben J. Hanson (MBS) eleza kwa kifupi madhara manne yanayoweza kutokea katika jamii iwapo itaendeleza mila potofu ya kuwabagua walemavu wa ngozi na pendekeza njia moja ambayo itazuia mila na desturi potofu.
8. Soma sehemu ya tamthiliya, kisha jibu maswali yanayofuata (Nyumbani kwa mwalimu Majaaliwa. Mama Onyango, Onyango na Tumaini wanaonekana. Mama yuko mezani anakunywa chai. Onyango amekaa kwenye meza ndogo anasoma na Tumaini anazunguka sebuleni akikimbiza gari lake la maboksi

ONYANGO: We, Tumaini acha kelele nitalitupa boksi lako nje.....Tulia

MAMA ONYANGO: Acha mwenzako acheze mbona wewe ulicheza, hakuna aliyekuzuia

ONYANGO: Mama si wewe ulikuwa ukitupa makopo yangu nje?

MAMA ONYANGO: Ndiyo lakini huo si ulikuwa uchafu ndani ya nyumba?

ONYANGO: Sasa huoni huyu nae anapiga kelele wakati mimi nasoma

MAMA ONYANGO: Sawa, hebu nenda ukachochea moto mboga iive haraka ubandike chungu motoni, kabla mlevi huyu hajarudi

ONYANGO: Mama huoni mimi nasoma, si uende wewe

MAMA ONYANGO: Tunabishana ee! Nenda haraka. Kusoma kusoma nini? Wee mtu wa shule kweli? Hebu fanya haraka (Onyango anainuka)

MAMA ONYANGO: Tumaini njoo baba nikupe chai

TUMAINI: Mimi sitaki chai nataka maziwa

MAMA ONYANGO: Maziwa tutayatoa wapi? Baba yako anaywea pombe hela zake. Na leo atanitambua

TUMAINI: Utamchapa? Na mimi nitamchapa mama (Onyango anaingia kutoka jikoni)

MAMA ONYANGO: Hivi Onyango baba yako alifika saa ngapi?

ONYANGO: Sijui

MAMA ONYANGO: Tumaini, baba yajo alienda dukani saa ngapi?

TUMAINI: Dumm Duu Duum pipipii, vuum anaona breki yangu mama!

MAMA ONYANGO: Muone masikio yake kama ya popo

BABA ONYANGO: Kifo000 kifo000

Kifo kinaua watu x 2

MAMA ONYANGO: Wewe mlevi hebu tuondolee kelele zako hapa (Anamsukuma mme wake)

BABA ONYANGO: (Anaacha kuimba na kuanza kutapika)

MASWALI

8. (a) Onesha tamathali za semi tatu zilizojitokeza katika sehemu ya tamthiliya uliyosoma
- (b) Vitendo vya baba na mama Onyango vina athari gani katika malezi ya watoto?
- (c) Taja mitindo miwili iliyotumika na mwandishi
- (d) Eleza namna mwandishi amemchora mama Onyango katika sehemu ya tamthiliya uliyosoma
- (e) Taja dhamira mbili zinazojitokeza katika tamthiliya hii

SEHEMU C (Alama 30)
Jibu maswali mawili tu katika sehemu hii
Swali la 9 ni la lazima

ORODHA YA VITABU

USHAIRI

Wasakatonge	-	Ms Khatibu (DUP)
Malenga wapya	-	TAKILUKI (DUP)
Mashairi ya Chekacheka	-	T.A Mvungi

RIWAYA

Takadini	-	Ben J. Hanson (NBS)
Watoto wa mama Ntilie	-	E. Mbogo
Joka la Mdimu	-	A. J. Safari

TAMTHILIYA

Orodha.....	-	Steve Reynolds
Ngoswe Penzi kitovu cha uzembe	-	E. Semzaba
Kilio chetu	-	Medical Aid Foundation

9. Umeagizwa na mwalimu wako wa kiswahili kutunga shairi moja utakaloghani siku ya mahafali yenu ya kuhitimu kidato cha nne. Lengo la shairi hilo ni kuwasaidia wahitimu kuboresha maisha yao ya baadae. Chagua mashairi matatu kwa kila diwani kutoka katika diwani mbili ulizosoma kisha eleza mafunzo utakayoyajumuisha katika shairi lako.
10. Wewe ni mchambuzi chipukizi wa kazi za fasihi. Onesha namna wahusika wanavyotumika kuibua kero mbalimbali katika jamii. Tumia wahusika watatu kutoka katika riwaya mbili ulizosoma
11. "Ugonjwa wa UKIMWI bado ni tishio kwa watanzania na dunia kwa ujumla. Kwa kutumia tamthiliya mbili ulizosoma onesha mambo yanayopelekea maambukizi ya UKIMWI kwa jamii kwa kutoa hoja tatu kwa kila kitabu